JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

______

# SHERIA YA MTOTO
[Sura ya 13]

## TAFSIRI YA KANUNI ZA UASILI WATOTO ZA MWAKA 2012

Toleo hili la Kanuni za Uasili wa Watoto za mwaka 2012, Tangazo la Serikali Na. 197 la tarehe 1 Juni, mwaka 2012, ni Tafsiri Rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Mbalimbali, Sura ya 1.

Dar es Salaam
28 April, 2016

George M. Masaju,
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 164 la tarehe 13/05/2016

SHERIA YA MTOTO

(SURA YA 13)

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UASILI

3. Kanuni za jumla.
4. Maombi ya kuasili mtoto.
5. Ridhaa ya kuasili.
6. Utenguaji wa ridhaa.
7. Kutohitaji ridhaa ya wazazi.
8. Kujibu maombi.
9. Umri wa mtoto.
10. Taarifa ya kusikilizwa kwa shauri.
11. Taarifa ya Uchunguzi ya Kijamii.
12. Masharti ya kuasili.
13. Amri ya kuasili.
14. Mahudhurio ya wahusika.
15. Maombi ya awali.
16. Usimamizi baada ya kuasili.
17. Usiri wa nyaraka na taarifa.
18. Rejesta ya kuasili.
19. Gharama.
20. Mtoto kupata kumbukumbu na taarifa na kuwasiliana na wazazi wake.

SEHEMU YA TATU
UASILI WA WAZI

21. Maombi ya Uasili wa Wazi.
22. Matokeo ya Uasili kwa Wazi.
23. Amri ya kuwasiliana katika Uasili wa Wazi.
24. Mtoto kufahamu juu ya uasili.

SEHEMU YA NNE
KUASILI KWA MTANZANIA ASIYEKUWA MKAZI

25. Maombi ya kuasili ya Mtanzania asiyekuwa mkazi.
26. Taarifa za ziada zinazohitajika kwa maombi ya Mtanzania asiyekuwa mkazi .

SEHEMU YA TANO
KUASILI KWA WAGENI

27. Maombi ya kuasili kwa raia wa kigeni.
28. Taarifa za ziada zinazohitajika kwa maombi ya raia wa kigeni.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

29. Matumizi ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai.

---

JEDWALI

---

SHERIA YA MTOTO
(SURA YA 13)

# KANUNI

## KANUNI ZA UASILI WATOTO
(*Zimetungwa chini ya kifungu cha 75, 157(c) na (9))*

## SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Kuasili Watoto, za mwaka 2012.

Tafsiri

**2.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama mukhtadha utahitaji vinginevyo -

Sura ya 13

"sheria" maana yake ni Sheria ya Mtoto;

"uasili" maana yake ni utaratibu wa kumpatia mtoto aliyekosa mazingira ya kifamilia kupata matunzo ya kudumu ya kifamilia;

"mtoto aliyeasiliwa" maana yake ni mtoto aliyeasiliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria;

"mzazi anayeasili" maana yake ni mtu ambaye amemuasili mtoto kwa mujibu wa masharti ya Sheria;

"muombaji" maana yake ni mtu au kikundi cha watu wanaoomba amri ya uasili;

"familia ya kuzaliwa" maana yake ni familia ya kibaiolojia ya mtoto;

"Mahakama" maana yake ni Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya ambako maombi ya kuasili yanafunguliwa;

"mtoto" maana yake ni mtu aliye na umri chini ya miaka 18 na ambaye amri ya uasili inaombwa au imetolewa;

"Mlezi" maana yake ni Afisa wa Ustawi wa Jamii aliyeteuliwa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii kuwakilisha haki za mtoto Mahakamani katika kipindi chote cha maombi ya kuasili;

"Jaji" maana yake ni Jaji wa Mahakama Kuu;

"Msajili" maana yake ni Msajili wa Mahakama Kuu na inajumuisha Kaimu Msajili, Naibu Msajili na Msajili wa Wilaya;

Sura ya 11

"Hakimu Mkazi' maana yake ni hakimu mkazi aliyeteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mahakimu wa Mahakama;

"Afisa Ustawi wa Jamii" maana yake ni Afisa Ustawi wa Jamii mfawidhi wa jiji anayefanya kazi ambaye yupo kwenye utumishi wa Serikali ni mkuu wa jiji, manispaa, mji au halmashauri ya Wilaya, kwa namna itakavyokuwa.

## SEHEMU YA PILI
### UASILI

Kanuni za jumla

**3.** Katika kufanya maamuzi yoyote kuhusiana na suala la kuasili mtoto, maslahi bora ya mtoto lazima yawe ndio kigezo kikuu na Mahakama maalum au chombo chochote cha umma-

(a) kitayakiainisha matakwa na hisia za mtoto;

(b) kitazingatia umri, kupevuka na uelewa wa mtoto;

(c) tazama kwa umakini namna ya kumuendeleza mtoto katika ukuaji, mila, kidini na kitamaduni.

(d) litajiepusha kuchelewa kufanya maamuzi juu ya maisha ya baadae ya mtoto; na

(e) kitahakikisha haimtenganishi mtoto na ndugu waliozaliwa tumbo moja na mtoto labda kama kuwatenganisha huko kutakuwa ni kwa maslahi bora ya mtoto.

Maombi ya kuasili mtoto

**4.**-(1) Mtu ambaye ana nia ya kuasili mtoto atafanya hivyo kwa njia ya maombi kama yalivyoainishwa katika Jedwali ambayo atayasajili katika masjala ya Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya.

(2) Maombi chini ya kifungu kidogo cha (1) yanaweza kufanywa na mtu binafsi au kwa ushirikiano kwa kuzingatia kifungu cha 56 cha Sheria.

(3) Maombi chini ya kanuni hii lazima yaambatanishwe na Cheti cha kuzaliwa, kadi ya utambulisho au nakala yoyote inayomtambulisha muombaji, cheti cha ndoa pale ambapo maombi yamefanywa na mume na mke, hati ya kiapo ya muombaji au waombaji.

(4) Muombaji atafanya maombi yeye binafsi au kwa kutumia Wakili kwa Jaji au Hakimu katika chumba cha kusikilizia kesi na Jaji au Hakimu atatoa maelekezo ya uwasilishwaji, uteuzi wa mlezi na idhini yoyote kama itakavyotakiwa.

(5) Kamishna atamteua Afisa wa Ustawi wa Jamii kusimama kama mlezi wa mtoto na ataitaarifu Mahakama kwa maandishi juu ya uteuzi huo.

(6) Kila maombi, taarifa au nyaraka isipokuwa kama Mahakama itaelekeza vinginevyo zitapelekwa na mpeleka wito wa Mahakama kwa mtu anaetakiwa kupelekewa wito huo kwa kuwasilisha nakala iliyosainiwa na Msajili au Hakimu Mfawidhi na kuwekwa lakiri ya Mahakama na upelekaji wa maombi yoyote, taarifa au nyaraka utathibitishwa kwa kiapo isipokuwa kama Jaji au Hakimu ataelekeza vinginevyo.

(7) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 56(3)(b) cha Sheria, mtu hawezi kuwasilisha maombi ya kuasili isipokuwa pale ambapo mtoto amekuwa chini ya uangalizi wa Muombaji kwa muda usiopungua miezi sita mfululizo kabla ya kufikiwa kwa tarehe ya maombi.

Ridhaa ya kuasili

**5.-**(1) Pale ambapo muombaji wa kuasili ana ridhaa ya maandishi kutoka kwa mzazi au mlezi, ridhaa hiyo itawasilishwa pamoja na maombi ya kuasili.

(2) Pale ambapo Mzazi hajatoa ridhaa kwa maandishi juu ya kuasili, Mahakama inaweza ikazingatia maombi na kuachana na ridhaa kwa mujibu wa kifungu cha 57(2) cha sheria, labda kwa suala lolote linaloangukia chini ya kanuni ya 50 ya Kanuni za Ulinzi wa mtoto, Mahakama haitahitaji ridhaa ya mzazi.

(3) Pale ambapo maombi ya kuasili yamefanywa kuhusiana na mtoto mwenye umri wa miaka kumi na nne na amepevuka vya kutosha kuelewa maana na matokeo ya kuasili, ridhaa ya mtoto huyo italazimika kupatikana kabla ya amri ya kuasiliwa kutolewa.

(4) Ridhaa chini ya kanuni hii lazima iwe kwa maandishi na kusainiwa mbele ya Kamishna wa viapo au afisa na Ubalozi pale ambapo ridhaa imetolewa nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(5) Kamishna wa Viapo au Afisa Ubalozi ambaye ridhaa imesainiwa mbele yake atalazimika kumtaarifu mtu aliyetoa ridhaa hiyo kuhusiana na matokeo ya kuasili na haki ya kutengua ridhaa hiyo ndani ya siku sitini kuanzia tarehe ya kutolewa kwa ridhaa hiyo.

(6) Ridhaa chini ya kanuni hii inatakiwa kuwa katika mfumo kama ulivyoainishwa katika Fomu M3 kama inayoonekana katika Jedwali.

Utenguaji wa ridhaa

**6.** Mtu ambaye ametoa ridhaa yake kulingana na masharti ya Sheria na Kanuni hizi anaweza kutengua idhini yake mbele ya kamishna wa viapo au Afisa wa Ustawi wa Jamii ndani ya siku sitini tokea tarehe ya kutolewa ridhaa hiyo kwa mfumo kama ulivyoainishwa katika Fomu namba 4 na 5 kama zinavyoonekana katika Jedwali.

Kutohitaji ridhaa ya wazazi

**7.-**(1) Mahakama inaweza kutohitaji ridhaa ya wazazi kulingana na masharti ya kifungu cha 57(2) cha Sheria, pale ambapo-

(a) mtoto ametelekezwa au anateswa na wazazi;

(b) wazazi hawajulikani walipo;

(c) mzazi au wazazi hawana uwezo na kutoa ridhaa au ridhaa imekataliwa bila sababu za msingi na mzazi mmoja au wazazi wote wawili.

(2) Mahakama itazingatia-

(a) uchunguzi wowote wa kijamii au Ripoti ya Upelelezi iliyoandaliwa juu ya mtoto na makadirio yoyote yaliyofanywa juu ya mtoto na wazazi yaliyoandaliwa na Afisa wa Ustawi wa Jamii katika eneo lolote ambalo mtoto anaishi au aliwahi kuishi.

(b) uonevu au unyanyasaji wowote uliofanywa dhidi ya mtoto na wazazi wake;

(c) kipindi ambacho mtoto alikuwa akipata uangalizi nje ya familia yake na mawasiliano ya mara kwa mara kati ya mtoto na wazazi katika kipindi hicho.

(3) Mahakama katika kuamua kama mzazi hawezi kupatikana itahakikisha ya kwamba uchunguzi wa kutosha umefanywa juu ya wale wanaoweza kujua mahali mzazi anapoishi ikijumuisha wanafamilia na Mwajiri wake wa mwisho kufanya kazi kwake anayejulikana.

(4) Mahakama katika kufanya maamuzi kama mtu hana uwezo wa kutoa ridhaa itazingatia-

(a) kama mzazi ana uwezo wa kutoa ridhaa; na

(b) kipindi ambacho mzazi amekosa uwezo ikitilia maanani umuhimu wa mtoto kukulia ndani ya familia aliyozaliwa.

(5) Mahakama katika kufanya maamuzi iwapo idhini imekataliwa bila sababu za msingi itazingatia-

(a) haki ya mtoto kukua katika mazingira ya kifamilia;

(b) mahitaji ya mtoto kuwa na familia mbadala ya kudumu;

(c) ukaribu wowote uliopo kati ya mtoto na familia ya mwombaji na familia yake alikozaliwa; na

(d) uwezekano wa mtoto kujumuika na familia yake alikozaliwa katika muda ambao uko katika maslahi bora ya mtoto.

(6) Mahakama katika kufikia maamuzi juu ya kuachana na ridhaa ya mzazi itazingatia ripoti ya Afisa wa Ustawi wa Jamii aliyeteuliwa na pamoja na hayo itachukua ushahidi wa maneno kutoka kwa Afisa wa Ustawi wa Jamii kulingana na maslahi bora ya mtoto.

(7) Mahakama katika kufikia uamuzi juu ya kutohitaji ridhaa ya mzazi itazingatia ya kwamba uchelewaji wowote wa kufanya maamuzi kuhusiana na malezi ya mtoto unaweza ukathibitishwa kama ulifanywa kwa maslahi bora ya mtoto.

Kujibu maombi

**8.** Mtu ambaye ridhaa yake inahitajika na sheria anaweza kuwasilisha hati ya kiapo katika kujibu maombi.

Umri wa mtoto

**9.-**(1) Umri wa mtoto utathibitishwa kwa kuiridhisha Mahakama ambayo itachukua nakala au ushahidi mwingine katika kuamua umri wa mtoto.

(2) Nakala iliyothibitishwa iliyoingizwa katika rejesta ya Vizazi na Vifo na mtu aliyeteuliwa chini ya Sheria ya Usajili ya Vizazi na Vifo kuhusiana na mtoto itakuwa ni ushahidi kutokana na maelezo yanayopatikana ndani yake.

(3) Mahakama yenyewe itafanya uchunguzi juu ya umri wa mtoto na inaweza kutoa amri ya mtoto kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu.

(4) Hati iliyosainiwa na Afisa tabibu kuhusiana na umri wa mtoto itachukuliwa kama ushahidi wa umri wake.

Taarifa ya kusikilizwa kwa shauri

**10.-**(1) Msajili au Hakimu Mfawidhi atateua pale ambapo nyaraka zote zimewasilishwa kwa namna itakayoridhisha Mahakama na Afisa wa Ustawi wa Jamii aliyeteuliwa na Mahakama kuwa mlezi, siku ya kusikiliza maombi na kutoa notisi katika mfumo ulioainishwa katika Fomu Namba Sita kama inavyoonekana katika Jedwali kwa wahusika ikijumuisha Afisa wa Ustawi wa Jamii na siku aliyoteuliwa na notisi hiyo itatolewa kwa wahusika wote kwa muda usiopungua siku saba kabla ya siku iliyopangwa kwa ajili ya kusikiliza shauri.

(2) Jaji au Hakimu wakati anasikiliza maombi ya kuasili atakaa faragha na hatasikiliza shauri jingine lolote katika kipindi hicho.

Taarifa ya Uchunguzi wa Kijamii

**11.-**(1) Afisa wa Ustawi wa Jamii ataandaa Taarifa ya Uchunguzi ya Kijamii kwa mujibu wa kifungu cha 75(2) cha sheria kuisaidia Mahakama kuamua kama kuasili huko ni kwa maslahi bora ya mtoto.

(2) Taarifa iliyoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) itawasilishwa mahakamani katika mfumo ulioainishwa katika fomu namba saba inayoonekana katika Jedwali.

(3) Taarifa ya uchunguzi wa kijamii itajumuisha taarifa zinazojitosheleza kuhusiana na jitihada zilizofanywa za kumuunganisha mtoto na wazazi wake wa kumzaa na makadirio yaliyofanyika ya namna ya kumuunganisha mtoto na familia yake ya kuzaliwa ndani ya muda mwafaka uliowekwa.

(4) Taarifa ya uchunguzi wa kijamii itajumuisha taarifa kuhusiana na ndugu waliozaliwa tumbo moja na mtoto.

(5) Afisa wa Ustawi wa Jamii atafanya makadirio kama kuasili ni kwa maslahi bora ya mtoto akizingatia kwa upana uwezekano wa mtoto kuungana na familia yake alikozaliwa ndani ya muda ambao ni kwa maslahi bora ya mtoto.

(6) Afisa Ustawi wa Jamii atafanya makadirio ya ujumla juu uwezo wa wazazi kuasili na kama wana uwezo wa kuasili mtoto ambaye ni mhusika katika maombi ya kuasili.

(7) Afisa Ustawi wa Jamii atahakikisha kwamba mawazo ya mtoto kuhusiana na kuasili yanahakikiwa na kurekodiwa katika taarifa ya upelelezi ya kijamii.

(8) Afisa wa Ustawi wa Jamii atamueleza mtoto juu ya matokeo ya kuasili ili aweze kuhakiki mawazo ya mtoto na uelewa wake.

(9) Afisa wa Ustawi wa Jamii atatazama kwa makini maslahi bora ya mtoto na muda wote atawakilisha maslahi ya mtoto.

(10) Mtazamo juu ya Watoto wa Muombaji wanaoishi lazima uzingatiwe ili kuweza kuamua kama kuna uwezekano wa kuasili au la.

(11) Katika kuhakiki uwezo wa muombaji na uwepo wa watoto wake, Afisa wa Ustawi wa Jamii atatembelea nyumbani kwa Mwombaji.

(12) Pale ambapo taarifa ya uchunguzi ya kijamii itaandaliwa na mtu mwingine au Mamlaka ya Serikali za Mitaa, nakala ya taarifa ripoti hiyo itawasilishwa kwa Afisa wa Ustawi wa Jamii ambae ataipitia taarifa hiyo na kutoa mrejesho kwa Mahakama.

(13) Afisa wa Ustawi wa Jamii katika kuongezea katika taarifa iliyotolewa katika taarifa ya uchunguzi wa kijamii atatoa-

(a) taarifa za nyuma za Muombaji ikijumuisha na kumbukumbu zozote za uhalifu;

(b) taarifa ya kitabibu ikielelezea hali ya afya ya mwombaji; na

(c) taarifa ya kitabitu ikielezea hali ya afya ya mtoto na pale itakapoonekana inafaa, maelezo juu ya mahitaji yoyote muhimu ya mtoto.

Masharti ya kuasili

**12.-**(1) Pale ambapo muombaji wa amri ya kuasili yuko juu ya umri wa miaka hamsini , Mahakama itaamua juu ya uwezo wa muombaji kuasili mtoto ikizingatia umri wa mtoto anayeasiliwa kwa kuzingatia kuwa iwapo mtoto yuko chini ya umri wa miaka kumi basi uasili hakutakuwa katika maslahi bora ya mtoto iwapo kama imefafanuliwa vinginevyo kwa umakini katika taarifa ya uchunguzi ya kijamii iliyoandaliwa na Afisa wa Ustawi wa Jamii.

(2) Mtu au familia haitaruhusiwa kuasili watoto zaidi ya watatu kwa wakati mmoja kwa kuzingatia kuwa Mahakama, inaweza kutokana na msingi wa kila shauri kuruhusu kuasili watoto zaidi ya watatu kwa mtu mmoja au familia kwa wakati mmoja kama itathibitishwa na Mahakama hiyo kuridhika kuwa ni katika maslahi bora ya mtoto kwa Muombaji kuasili watoto zaidi ya

watatu.

Amri ya kuasili

**13.-**(1) Mahakama, baada ya kusikiliza maombi ya kuasili na kuridhika kwamba kuasili kwa mtoto ni katika maslahi bora ya mtoto huyo na muombaji anaweza kuasili, itatoa amri ya kuasili kwa utaratibu ulioainishwa katika Fomu Namba Tisa inayoonekana katika Jedwali.

(2) Nakala ya amri iliyotolewa na Mahakama haitatolewa au kupewa kwa mtu yeyote zaidi ya Muombaji na Msajili Mkuu isipokuwa kama Mahakama itaelekeza vinginevyo.

(3) Amri ya kuasili haitatolewa mpaka kumalizika kwa muda wa nyongeza na siku sitini wa mtoto au mzazi kuondoa ridhaa zao kama inavyoelekezwa katika kanuni ya 5.

(4) Pale ambapo amri ya kuasili haijatolewa hali ya malezi ya mtoto kama ilivyokuwa kabla ya kuasili itazingatiwa isipokuwa kama Mahakama itaelekeza vinginevyo au pale ambapo Afisa Ustawi wa Jamii ataamua kusitisha kuamishwa kwa mtoto huyo.

Mahudhurio ya wahusika

**14.-**(1) Wahusika katika maombi watahudhuria mbele ya mahakama pale shauri litakapoitwa kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

(2) Mahakama kabla ya kutoa amri ya kuasili au ya muda, itataka wahusika wote kuhudhuria au kutoa amri pasipo wao kuwepo hawapo na itatoa amri kwamba kila muhusika ahudhurie mbele yake peke yake kwa ajili ya usaili.

Maombi ya awali

**15.** Pale ambapo kuna ushahidi kuwa mwombaji muombaji alifanya maombi hapo awali kuhusiana na uasili wa mtoto na maombi hayo yakakataliwa, Mahakama haitatoa amri ya kuasili au amri ya uasili ya muda isipokuwa kama itajiridhisha kuwa kuna mabadiliko makubwa ya msingi ya kimazingira .

Usimamizi baada ya kuasili

**16.-**(1) Afisa Ustawi wa Jamii atafanya ziara ya ufuatiliaji katika nyumba ya wazazi walioasili miezi mitatu baada ya Amri ya kuasili kutolewa na Mahakama iwapo wazazi walioasili wanaishi Tanzania.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii wakati wa ziara ya ufuatiliaji atakutana na mtoto kwa faragha akitilia maanani umri wa mtoto, ukomavu na hatua ya ukuaji, ushawishi wa maoni ya mtoto juu ya kuasili.

(3) Afisa Ustawi wa Jamii ataandika taarifa kkuhusu ziara ya ufuatiliaji huo na kuiweka katika jalada la mtoto.

(4) Ulinzi wowote wa mtoto husika utashughulikiwa kama ilivyoainishwa katika sheria.

(5) Pale ambapo wazazi walioasili wanaishi nje ya Tanzania, Kamishna kwa kushauriana na huduma za Jamii za Kimataifa watafanya ufuatiliaji baada ya uasili kwa ajili ya kuhakikisha ya kwamba mtoto analindwa hata baada ya kuasiliwa.

(6) Kamishna kila baada ya muda atatengeneza miongozo ya usimamizi wa mtoto ambaye tayari ameasiliwa.

Usiri wa nyaraka na taarifa

**17.-**(1) Nyaraka zote zitakazosajiliwa Mahakamani zitachukuliwa kuwa za siri na kutunzwa kwa siri na Msajili isipokuwa pale Msajili isipokuwa kwa maombi anaweza akatoa nakala hizo na kuweza kupatikana kwa mtu yeyote.

(2) Afisa wa Ustawi wa Jamii atachukua taarifa zote zitakazopatikana wakati wa upelelezi au kwa namna yoyote kuhusiana na jambo hilo kama siri na hatatoa sehemu yoyote taarifa hizo kwa mtu yoyote isipokuwa kama italazimika kwa utendaji mzuri wa majukumu yake.

Rejesta ya kuasili

**18**.-(1) Msajili wa Mahakama Kuu kwa mujibu wa kifungu cha 69(2) na (3) cha Sheria atawasilisha nakala halisi za vitu vifuatavyo kwa Msajili Mkuu-

(a) Amri ya kuasili;

(b) mwenendo wa shauri wa Mahakama kuhusiana na shauri la kuasili; na

(c) nakala au taarifa yeyote muhimu kama Msajili atakavyoona inafaa.

(2) Msajili Mkuu baada ya kupokea nakala zilizoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), atazisajili nakala hizo katika rejesta ya kuasili.

(3) Afisa Ustawi wa Jamii ambaye atateuliwa kama Mlezi na Mahakama kwa ajili mlolongo wa zoezi la kuasili atamtaarifu kamishna juu ya kuasili na atatoa nakala za amri ya kuasili kwa Kamishna na kuweka nakala ya amri ya kuasili katika Jalada la mtoto.

Gharama

**19.** Mahakama inaweza kutoa amri juu ya gharama kama Jaji au Hakimu atakavyoona inafaa na Mahakama itaelekeza ya kwamba gharama zote za maombi chini ya sheria zitabebwa na kulipwa na muombaji.

Mtoto kupata kumbukumbu na taarifa na kuwasiliana na wazazi wake

**20.**-(1) Mtoto aliyeasiliwa ataruhusiwa kupata taarifa zinazohusiana na kuasiliwa kwake muda wowote baada ya kufikia umri wa miaka kumi na nne.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii atafanya jitihada za kutoa taarifa juu ya mazingiara ya kuasili isipokuwa pale itakapochukuliwa ni kinyume na maslahi bora ya mtoto.

(3) Afisa wa Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wazazi walioasili watachukua hatua za msingi za kumsaidia mtoto aliyeasiliwa kuwasiliana na familia yake alikozaliwa na kwa kufanya hivyo Afisa wa Ustawi wa Jamii atazingatia kama wazazi waliomzaa wanahitaji kuwasiliana kwa kuchukulia mazingira ya kuasili huko na kama kuwasiliana huko ni kwa maslahi bora ya mtoto.

## SEHEMU YA TATU
### UASILI WA WAZI

Maombi ya Uasili wa Wazi

**21**(1) Mtu ambaye ana nia ya kuasili mtoto ambaye ni ndugu yake atatekeleza taratibu kama zilivyoelekezwa katika Kifungu cha 54(1)(b) cha Sheria.

(2) Mwenendo wowote na masharti yaliyotolewa chini ya Sheria au Kanuni hizi kuhusiana na uasili mtoto yatalazimika kufuatwa na mwombaji wa kuasili

Matokeo ya Uasili wa Wazi

**22.** Amri ya uasili wa wazi itakuwa na matokeo sawa na kule kuasili kunakofanywa chini ya kifungu cha 54 cha Sheria isipokuwa kwa kiasi fulani -

(a) ukaribu kati ya familia aliyozaliwa na mtoto anayeasiliwa utunzwe; na

(b) hakutakuwa na kubadilika kwa jina la mtoto la familia labda wazazi wanaomuasili, familia alikozaliwa na mtoto anayeasiliwa wakubaliane.

Amri ya kuwasiliana katika Uasili wa Wazi

**23.**-(1) Mahakama ikijumuisha pamoja na amri iliyotoa inaweza kutoa maelekezo ya kwamba, familia ya mtoto alikozaliwa kuonana na kuwasiliana na mtoto alieasiliwa ili kudumisha ukaribu wao labda kama kuwasiliana huko sio kwa maslahi bora ya mtoto.

(2) Pale ambapo Mahakama itakapotoa Amri ya kuwasiliana kama inavyoelezewa katika kifungu kidogo cha (1), wazazi walioasili wataruhusu mawasiliano hayo kama watakavyokubaliana au kuainishwa katika amri.

Mtoto kufahamu juu ya uasili

**24.** Bila kuathiri kifungu cha 61 cha Sheria, kwa kuzingatia asili ya uasili kwa uwazi, wazazi walioasili wanaweza kuchagua kumtaarifu mtoto juu ya kuasiliwa kwake na ukoo wake kabla mtoto hajatimiza umri wa miaka kumi na nne ikiwa kufanya hivyo hakutakuwa ni kinyume na maslahi bora ya mtoto.

## SEHEMU YA NNE
### KUASILI KWA MTANZANIA ASIYEKUWA MKAZI

Maombi ya kuasili ya Mtanzania asiyekuwa mkazi

**25.** Raia wa Tanzania ambaye si mkazi na anania ya kuasili mtoto atafuata taratibu za maombi na masharti ya maombi ya kuasili kama yalivyoelekezwa chini ya Sheria na kanuni hizi.

Taarifa za ziada zinazohitajika kwa maombi ya Mtanzania asiyekuwa mkazi

**26.** Afisa wa Ustawi wa Jamii akijumuisha na taarifa zinazotakiwa katika Taarifa ya Upelelezi ya kijamii atahakikisha ya kwamba Mahakama imepatiwa taarifa zifuatazo:

(i) makadirio yaliyofanywa na Mamlaka inayotambulika kule ambapo muombaji anaishi na pale itakapohitajika kutoka nchi yake ya asili, juu ya uwezo wa muombaji kuasili; na

(ii) maelezo kuhusiana na taarifa zozote za kihalifu za muombaji ikijumuisha makosa ya kihalifu kuhusiana na udhalilishaji wa mtoto katika nchi alikozaliwa na kama muombaji anaishi nje ya nchi alikozaliwa basi nchi anayoishi.

## SEHEMU YA TANO
### KUASILI KWA WAGENI

Maombi ya kuasili kwa raia wa kigeni

**27.** Mgeni mwenye nia ya kuasili mtoto atafuata taratibu na masharti ya maombi ya kuasili mtoto kama yalivyoelekezwa katika Sheria na Kanuni hizi.

Taarifa za ziada zinazohitajika kwa maombi ya raia wa kigeni

**28.** Ikijumuisha na taarifa zinazotakiwa katika taarifa ya kipelelezi wa Kijamii, Afisa wa Ustawi wa Jamii atahakikisha Mahakama imepatiwa vitu vifuatavyo:

(a) taarifa za uhakika kuhusiana na jitihada zilizochukuliwa kumpatia mtoto malezi sahihi ndani ya Tanzania;

(b) makadirio ya Mamlaka inayotambulika kule Muombaji anakoishi na kama itakavyoonekana inafaa, kutoka katika nchi alikozaliwa juu ya uwezo wa muombaji kuasili;

(c) maelezo kuhusiana na lugha ya muombaji, utamaduni, jamii na dini; na

(d) maelezo kuhusiana na rekodi zozote za uhalifu za muombaji ikijumuisha makosa ya kihalifu ya udhalilishaji wa mtoto katika nchi alikozaliwa na kama muombaji anaishi nje ya nchi alikozaliwa basi kutoka katika nchi anakoishi.

## SEHEMU YA SITA
### MASHARTI YA JUMLA

Matumizi ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai

**29.** Masharti ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai itatumika katika taratibu chini ya Sheria pale itakapoonekana zinaweza kutumika.

____

**JEDWALI**

_____

FOMU

FOMU NA. AC.I

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA UASILI WA WATOTO ZA MWAKA 2015

(T.S.Na. ................ la mwaka 2015

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA/HAKIMU MKAZI/MAHAKAMA KUU* YA TANZANIA

Katika suala la Sheria ya Mtoto, na suala la A.B (jina la mtoto mwasiliwa) wa …………............... ........................................................................................................................................... (anwani)

Maombi ya C.D (jina la mwombaji) wa ............................................................................................ .............................................................................................................................. (anwani)

(na E.D. jina la mke/mume wa mwombaji wa anwani sawa na mwombaji)

1. Mwombaji anataka/waombaji wanataka kumuasili mtoto anaitwa A.B. chini ya vifungu vya Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

2. Mwombaji au waombaji ni mkaazi/wakaazi wa …….............................................. katika mkoa wa ................................................................ Tanzania**

3. Mwombaji C.D. hajaoa/hawajaolewa (ameoa/ameolewa na E.D katika .................. tarehe ...........................................

4. Mwombaji C.D. ni ............................................................................... (kazi anayofanya.)

5. Mwombaji C.D. ana umri wa miaka ........................................ na mwenza wa mwombaji E.D. ana umri wa miaka .......................................................

6. Mwombaji/waombaji wanaoishi pamoja na watu wafuatao-

   Jina X.D (mtoto wa kiume) wa umri wa miaka jina .............................................

   Jina Y.D (mtoto wa kike) wa umri wa miaka .......................................................

7. Mwombaji C.D. (E.D.) wana uhusiano na AB ufuatao .................................................. mwombaji/waombaji miongoni mwao hakuna mwenye uhusiano wa aina yeyote na A.B.

8. Mtoto muasiliwa A.B –

   (a) Ni wa jinsia ya .................................

   (b) Ni raia wa ..........................................

   (c) Ni raia wa ..........................................

   (d) Ni mtoto wa .......................................................................................... (jina) wa ....................................................... (anwani)

   (e) .................................................................................................................. sababu za kuasili.

   (f) ............... umri ambaye ni mzaliwa wa ......................... tarehe ......................

   (g) Mwenyeji/mkaazi wa ....................................................................... (anwani)

   (h) Kwa sasa akiwa chini ya uangalizi wa ................................ (jina na anwani)

   (i) Mtoto anayeasiliwa anaishi katika kituo cha malezi ya watoto cha ................ ............................................................................................ (jina na anwani)

   (j) Mtoto anayeasiliwa ana haki ya mali zifuatazo ............................................ zilizopo eneo la ........................................................................................ (anwani, na ..................................................................................................... zilizopo eneo la ..................................................................................................... (anwani) ambazo zitatumika katika kuchangia kumsaidia huyo mtoto.

9. Mtoto anayeasiliwa (A.B) hajawahi kuasiliwa na mtu mwingine yeyote na wala hamna maombi ya mtu yeyote mwingine ya kutaka kumuasili hayo mtoto (eleza amri au maombi kama yapo).

10. Mwombaji (anayeasili) endapo maombi yatakubaliwa, utatakiwa kupata dhamana ya Mahakama au vinginevyo kama mahakama itakavyoelekeza.

11. Ridhaa ya maombi imepatikana kutoka kwa watu wafuatayo**

    (a) wazazi wa mtoto;
    (b) mlezi;
    (c) mtu ambaye ndiye anayemtunza huyo mtoto;
    (d) mtu/watu wanaohusika katika kuchangia kumsaidia mtoto;
    (e) mwenza wa mwombaji

(f) mtoto mwenyewe (endapo atakuwa na umri wa zaidi yamiaka 14).

12. Wewe mwombaji (waombaji) huja/hamja/wote kwa pamoja) pokea au kukubali kupokea na hakuna mtu yeyote ametoa au amekubali kutoa kwa mwombaji/waombaji (au mmoja kati yao) malipo yeyote au zawadi kwa ajili ya kumuasili mtoto aitwaye A.B (isipokuwa kama ifuatavyo)..................................................................................................... ......................................................................................................................................

13. Inapendekezwa kuwa gharama za maombi haya zitalipwa na .............................. ......................................................................................................................

Mwombaji anaomba kama ifuatavyo-

(a) Kwamba amri ya kumuasili mtoto A.B kutokana na maombi ya mwombaji/ waombaji iweze kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ikiwa ni pamoja na maelekezo yote muhimu;

(b) Kwamba gharama za maombi haya zinaweza kutolewa kama ilivyoelekezwa hapo juu au kwa namna mahakama itakavyoelekeza;

(c) Amri nyingine yeyote kwa namna mwenendo wa maombi haya utakavyoonekana inafaa.

**Tanbihi:** Inatarajiwa kuwasilisha maombi haya tarehe ........................................

* Futa ambacho hakihitajiki
** kwa waombaji wasio raia wa Tanzania, onyesha mahali na makazi yao ipasavyo.

SHERIA YA MTOTO

FOMU NA. A.C2

KANUNI ZA UASILI WA WATOTO ZA MWAKA 2015
(T.S.NA. .............................. LA MWAKA 2015)

KIAPO CHA KUTHIBITISHA MAOMBI

1. Kwamba masuala yaliyoelezwa katika kipengele cha 1 hadi cha 7 cha maombi ni ya kweli na ninayajua kwa akili yangu. Kwa upande wa umri wangu (na umri na mwombaji mwenza wangu E.D) angali nakala za hati za kuzaliwa zilizoambatishwa na kiapo hici, na pia angalia nakala ya hati ya ndoa ambayo imeambatishwa.

2. Masuala yaliyoelezwa katika kipengele cha 8(a)(b)(c), (g) na (h) cha maombi ni ya kweli na nina uchakika nayo kwa uelewa wangu. Masuala yaliyoelezwa katika vipengele vya (d), (e), (f), (i) na (j) ya maombi yangu kwa uelewa wangu ni kutokana na taarifa nilizozipata kutoka kwa ........................................................................................................ ........................................................................................................................................ wa .......................................................................................... na naamini kuwa ya kweli. Naambatisha hati ya kuzaliwa ya mtoto anayeombewa kuasiliwa (AB).

3. Uelewa wangu na taarifa zilizopo katika kipengele cha 8 ni kutokana na taarifa nilizozipata kutoka kwa ......................................................................................... na ........................................................................................................................................ na naamini kuwa za kweli.

4. Masuala yaliopo kwenye kipengele cha 9 cha maombi ni ya kweli kwa kadri ya uelewa, taarifa na imani yangu.

5. Masuala yaliyopo katika vipengele vya 11 na 12 ya maombi ni ya kweli na ninayojua kwa kadri ya uelewa wangu. Naomba nirejee ridhaa ya-
   (a) ............................................................ na ........................................... (wazazi)
   (b) ............................................................................................................... (mlezi)
   (c) .................................................................................. (mlezi wa kweli wa mtoto)
   (d) ........................................................................................ mtu/watu wanaohusika katika kuchangia kumsaidia mtoto)
   (e) ......................................................................... (mwenza wa mwombaji ambayo imeambaatishwa hapa.

______________________________

SHERIA YA MTOTO

FOMU NA. A.C3

KANUNI ZA UASILI WA WATOTO ZA MWAKA 2015
(T.S.NA. .............................. LA MWAKA 2015)

RIDHAA YA KUMUASILI MTOTO

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 7(2))*

(Jina kama ilivyo kwenye maombi) na katika maomi ya ..................................................................... ..................................................................................................................................... kwa ajili ya amri ya kumuasili ......................................................................................... (ambaye ni mtoto)

Mimi ambaye ni ........................................................... wa …............................................... nikiwa ni:

(a) baba mzazi wa mtoto;
(b) mama mzazi wa mtoto;
(c) Kamishna wa Ustawi wa Jamii;
(d) mlezi wa mtoto;
(e) mhusika ambaye ninaye wajibika katika kumsaidia huyu mtoto;
(f) mwenza wa mwombaji; na
(g) mtoto.

naeleza kwamba, naelewa mazingira na madhara ya amri ya kuasili mtoto ambayo imeombwa (na kwa uhakika zaidi najua madhara ya amri hiyo itaninyanganya haki yangu ya kukosa wazazi wangu wa kunizaa*. Nakubaliana na maombi yaliyowasilishwa ya kuomba amri ya kuasili kwa upande wa mwombaji/waombaji.

Kwa ushahidi, naweka saini hii ridhaa leo tarehe .............................. mwezi ......................., 20...
.......................................................................................................................... (anwani/makazi).
.......................................................................................................................... (saini)
Imesainiwa na ........................................................... mbele yangu baada ya kumfahamisha maana na madhara ya kuridhia na amri ya kuasili, na yeye ameonyesha kuelewa.

.......................................................................................................................... (saini ya shahidi)
Anwani .........................................................................................................................................
...................................................................................................................................................
...................................................................................................................................................
Mahusiano ....................................................................................................................................
...................................................................................................................................................
...................................................................................................................................................

* Hii inatumika kwa mtoto aliye na haki ya wazazi wa kumzaa tu.

SHERIA YA MTOTO

FOMU NA. A.C4

KANUNI ZA UASILI WA WATOTO ZA MWAKA 2015
(T.S.NA. ............................... LA MWAKA 2015)

KUJIONDOA KWA MZAZI AU MLEZI KATIKA
RIADHAA YA KUMUASILI MTOTO

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 9(1))*

KWA: JAJI/HAKIMU ANAYESIKILIZA
KUASILI KWA: (Jina kamili la mtoto)
NA: *(Majina ya wanaopendekezwa kuwa wazazi wa kuasili (watu) nisio wafahamu)
WA: (Wilaya ambamo maombi yamefanyika)

TAFADHALI NATAHADHARISHA KWAMBA:

